

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.



TAARIFA KWA UMMA

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Benjmini Kawe Sitta leo amezindua rasmi zoezi la ulipaji wa fidia awamu ya kwanza kwa wakazi **179** waliokamilishiwa taratibu za kihasibu na kuwasilisha nyaraka zao na akaunti zao za benki baada ya Serikali kutoa idhini ya ulipwaji wa fidia katika barabara za Makanya, Tandale-Kisiwani, Kilongawima , na Simu 2000 wanao athiriwa na mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika jiji la Dar es Salaam (**Dar es Salaam Metropolitan Development Project**).

Utekelezaji Wa mradi huu ulisimama katika baadhi ya maeneo kutokana na kukosa fedha za kulipia fidia, na sasa utaanza kutekelezwa katika maeneo hayo yaliyopata idhini kwa sasa huku ikisubiriwa idhini ya malipo katika barabara za Kilungule na Kilimani ili malipo yaweze kukamilika na miradi hiyo kutekelezwa kwa ufanisi na kwa ubora unaotakiwa katika barabara zote zinazohitaji kulipiwa fidia.

Utekelezaji wa mradi huu unafanywa kwa kwa awamu kulingana na mpango wa manunuzi (procurement plan) uliokubaliwa kati ya Benki ya Dunia ,na Serikali kuititia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Halmashauri ya ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 miradi iliyoanza kutekelezwa ni ya ujenzi wa barabara tano za awamu ya kwanza ambazo hazikuhitaji fidia kati ya barabara kumi na moja zinazotakiwa kujengwa ambazo ni Makumbusho-Sokoni, MMK, Nzasa, Tanesco – Soko la Samaki, na barabara ya viwandani.

Mradi huu unatekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam ukihusisha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa za Ilala , Kinondoni, Temeke na Ubungo ukiwa na lengo la kuboresha miundombinu, na kuzijengea uwezo katika utoaji wa huduma na kuungeza mapato .

Kazi zinazofanyika katika mradi huu zinahusisha maeneo muhimu kama ujenzi wa barabara zitakazopunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam (**Local Roads**), uboreshaji wa miundombinu katika makazi yasiyopangwa (**Infrastructure Upgrading in unplanned Settlements**), kuboresha mifereji ya maji ya mvua(**storm**